# MCHANGO WA TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI (TATAKI)[1] KATIKA KUKUZA NA KUENDELEZA UWANJA WA FASIHI YA KISWAHILI YA WATOTO NDANI NA NJE YA TANZANIA (2009-2016)

*L.H. Bakize*[2]

IKISIRI

Mwaka 2009, TATAKI, kupitia Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, iliamua kuanzisha kozi ya Fasihi ya Watoto na Vijana (KF 203) baada ya kupata ushauri wa mwalimu ambaye alikuwa ameanza kufanya utafiti wa uzamivu kwenye uwanja wa fasihi ya watoto (Lyimo, 2014). Ilipofika mwaka 2010 kozi hii iliamuliwa iwe miongoni mwa kozi za Programu ya Shahada ya Kwanza katika Taaluma za Kiswahili (B.A. Kiswahili) kwa mwaka wa masomo 2010/2011. Kozi hii inalenga kuwapa wanafunzi maarifa na mbinu za kutambua, kuelewa, kuchambua na kuhakiki kazi za fasihi ya watoto na vijana kwa nadharia na vitendo. Kwa upande wa uchambuzi, kozi hii inawapa wanafunzi mbinu mbalimbali za uchambuzi na uhakiki wa fasihi ya watoto na vijana katika vitabu, vyombo vya habari, na vyombo vingine vya kidijitali (TATAKI, 2010a). Wakati kozi ya fasihi ya watoto na vijana inaanza, ilikuwa ni kozi kwa ajili ya wanafunzi wa B.A. Kiswahili. Hata hivyo mwaka 2012 ilifanywa kozi ya lazima kwa wanafunzi wote wanaosoma digrii ya Ualimu na wanaochukua somo la Kiswahili kama somo la kufundishia wanapokuwa katika semesta ya pili ya mwaka wa pili. Mpaka tunapoyakamilisha makala haya, kozi hiyo bado ni ya lazima kwa wanafunzi tuliowataja. Pia, ni kozi ya hitiari kwa wanafunzi wengine nje ya hao tuliowataja. Tangu kuanzishwa kwa kozi hiyo, kwa kukadiria, wanafunzi zaidi ya 4,000 waliosoma shahada ya Ualimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaama, wakisoma pia somo la Kiswahili, wameisoma. Aidha, makala 16 katika uwanja wa fasihi ya watoto yamechapishwa, tasnifu mbili zimeandikwa kwa kiwango cha Umahiri na tasnifu moja ya Uzamivu. Hivi leo, uwanja huo wa fasihi ya watoto umeanza kuchangamkiwa kwa kuwa sasa unakua kwa kasi kutokana na mahitaji ya kitaifa na kimataifa (Ngugi, 2015). Makala haya yanakusudia kutathmini mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja huu tangu mwaka 2009 mpaka 2016. Ili kufanikisha azma ya makala haya mkabala wa kihistoria utatumika katika kueleza hoja zetu.

*Maneno muhimu:***Mchango wa TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maendeleo ya uwanja wa fasihi ya watoto, fasihi ya Kiswahili ya watoto**

## 1.0 UTANGULIZI

Katika makala haya, dhana ya “Fasihi ya Kiswahili ya Watoto” kama taaluma, tutaitumia kwa maana ya taaluma inayojikita katika kuandika, kutafiti na kuchapisha kazi za kifasihi zilizoandaliwa na watu wazima au watoto kwa lengo la kusomwa au kutendwa na watoto. Kwa madhumuni ya makala haya, tutajadili mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja wafasihi ya watoto kwa njia mbalimbali. Makala haya yatakuwa na manufaa kadhaa ambayo, miongoni mwa

[1] Katika sehemu zitakazofuata tutakuwa tukitumia neno TATAKI.

[2] Mwandishi ni Mkufunzi Msaidizi katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wakati anaandika makala haya alikuwa ni mwalimu wa Kiswahili katika Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi, Chuo Kikuu cha Zimbabwe. Pia, alikuwa ni mwanafunzi wa Uzamivu wa uwanja wa fasihi ya watoto katika Idara ya Lugha za Kiafrika na Fasihi, Chuo Kikuu cha Zimbabwe.

mengine ni mosi, kuwasaidia wale wasioifahamu TATAKI kuifahamu kwa ufupi; pili, yatawasaidia wanataaluma wanaobobea katika fasihi ya Kiswahili ya watoto kupata walau usuli wa historia ya uwanja huu tangu mwaka 2011 mpaka sasa; tatu, kuwawezesha wanafunzi wanaobobea katika uwanja wa fasihi ya watoto kupata dokezo la machapisho ya TATAKI, hasa majarida, ili iwe rahisi kwao kuyafuatilia majarida hayo na kuyasoma; nne, kuwajuza wale wasiofahamu chochote kuhusiana na fasihi ya Kiswahili ya watoto wajue kwamba kuna uwanja wa kitaaluma unaoitwa fasihi ya Kiswahili ya watoto ambao kwa Tanzania, ulianza kufundishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa masomo 2011/2012 katika Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tano, kuwawezesha watafiti kufahamu mchango wa TATAKI katika kuukuza na kuuendeleza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Sehemu inayofuata tutafafanua methodolojia tuliyoitumia katika kupata taarifa za makala haya na mkabala tutakaoutumia katika kufafanua hoja zetu katika makala haya.

## 2.0 METHODOLOJIA NA MKABALA WA MAKALA

Makala haya yametokana na utafiti ambao tuliufanya kwa kukusanya data kwa nyakati tofautitofauti kuanzia mwaka 2009. Ukusanyaji wa data ulitumia njia kadhaa. Mosi, tulitumia mbinu ya ushuhudiaji na ushiriki. Mwandishi, amekuwa akishiriki katika mambo mbalimbali yanayoihusu TATAKI kwa nyakati tofauti. Mathalani, mwaka 2009 wakati TATAKI inazinduliwa na Waziri Mkuu wa Tanzania, wa wakati huo, Mh. Mizengo Kayanza Peter Pinda, katika ukumbi wa Nkrumah, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwandishi alikuwapo kama mshuhudiaji na mshiriki. Pia, wakati huo mwandishi alikuwa mwanafunzi wa Digrii ya Ualimu (*B.A. Education*) katika mwaka wa tatu wa masomo hayo. Pili, tangu mwaka 2010 mwandishi aliajiriwa na TATAKI na kuwa sehemu yake. Hivyo, mpaka sasa mwandishi ana miaka 7 ya uzoefu wa kushiriki katika shughuli za TATAKI. Tatu, wakati wa kuanzisha ufundishaji wa kozi ya fasihi ya watoto na vijana mwaka wa masomo 2011/2012 katika Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, mwandishi alishiriki kama mwalimu msaidizi wa kozi hiyo, na ilipofika mwaka 2013 aliifundisha kozi hiyo akiwa mwenyewe kwa miaka miwili mpaka mwaka 2015. Nne, mwandishi ameshiriki pia katika uandishi wa makala kadhaa katika uwanja huo kuanzia mwaka 2011 mpaka sasa, na mpaka sasa bado anaendelea. Aidha, mwandishi amekuwa akiwezeshwa na TATAKI kwa nyakati tofauti kushiriki makongamano ya kitaaluma ndani na nje ya Tanzania. Katika makongamano hayo, mwandishi amekuwa akiwasilisha makala ya fasihi ya watoto. Hivyo, tunaweza kusema kuwa kwa ushiriki na ushuhudiaji huo, uzoefu wake unatosha kabisa kuisemea TATAKI katika kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili ya watoto.

Mbinu nyingine iliyotumika katika kukusanya data za makala haya ni upitiaji wa nyaraka. Nyaraka hizo ni pamoja na majarida, vitabu, Mwongozo wa Programu ya Digrii ya awali ya Kiswahili (*B.A Kiswahili*) na Mwongozo wa Programu ya Digrii ya Umahiri (*M.A Kiswahili*). Zaidi ya nyaraka hizo, brosha ya TATAKI ya mwaka 2014/2015 ilitusaidia sana katika kupata historia fupi ya taasisi.

Tumeamua kuuzungumzia uwanja wa fasihi ya watoto kwa sababu ni uwanja ambao unaibukia na kuwavutia watafiti mbalimbali tofauti na hali iliyokuwa hapo awali. Pengine hii ni kutokana na mkazo katika haki za watoto ambazo zinasisitizwa na Umoja wa Mataifa (Ngugi, 2015). Kutokana na hali hiyo, mtoto amewekwa katika kizimba makinikiwa katika nyanja mbalimbali za haki za binadamu, jinsia, elimu, afya, vita, mazingira, utaifa, na mengine kama hayo. Sababu ya pili iliyotuvutia kuumakinikia uwanja huu ni hali ya dharau ambayo imekuwapo kwa muda mrefu kwamba uwanja wa fasihi ya watoto hauna jipya na hata wanaoumakinikia ni watu wasioweza mambo magumu (Dube, 2004-2006; Jose, & Thomas, 2007). Ingawa dharau hiyo imekuwapo kwa miaka mingi, lakini kuanzia miaka ya 1980 uwanja huu ulianza kuchangamkiwa na wataalamu wa fasihi kutoka ndani na nje ya Bara la Afrika (Muponde & Stein, 2004-2006). Wataalamu wengi wamekiri na kushuhudia kwamba uwanja huu ni mpevu kama nyanja nyingine tu. Tafiti zimeonyesha kwamba fasihi ya watoto inabeba mambo mazito kijamii tofauti kabisa na jinsi ilivyokuwa ikifikiriwa hapo awali (Muponde, 2005). Akieleza sababu za mvuvumko huo wa kumakinikia kwa uwanja wa fasihi ya watoto, Ngugi (2012) anadai kuwa miaka ya hivi karibuni, fasihi hii ya watoto imemakinikiwa barani Afrika kwa sababu ya kuwawezesha watoto katika kujitambua, kukuza usomaji, kukuza utamaduni wa Kiafrika, ujinsia, utaifa, na kadhalika.

Aidha, tumeamua kuujadili mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kwa sababu ni taasisi ambayo inafahamika kuwa kongwe zaidi duniani, hasa ikizingatiwa kwamba historia yake inaanzia kwenye Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki iliyoanza mwaka 1930. Pia, nchini Tanzania, uwanja huu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto umeanza kufundishwa katika taasisi iliyoteuliwa kabla ya taasisi nyingine nchini Tanzania.

Makala haya yatatumia mkabala wa kihistoria. Matukio na taarifa kadhaa muhimu zitafafanuliwa kwa kutumia mbinu au mkabala huu wa kihistoria. Sifa mojawapo ya historia kama taaluma ni kwamba si kila kilichotokea kinaandikwa au kusimuliwa. Historia huchota matukio ambayo pengine yanasadifu malengo au mtazamo wa mwandishi au pia mahitaji ya jamii andikiwa. Ndiyo kusema, mambo yatakayoelezwa katika makala haya ni yale tu ambayo yanalenga kuineemesha makala ili kukamilisha malengo yake muhimu. Hivyo, si mambo yote yanayoihusu TATAKI au fasihi ya watoto yataelezwa. Tutaeleza yale ya muhimu tu.

## 3.0 HISTORIA FUPI YA TATAKI

Historia ya TATAKI inaanzia mwaka 1930 ambapo ilikuwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ikijishughulisha na yafuatayo[3]:

a) Kusanifisha Kiswahili kinachotumika katika shughuli rasmi katika Afrika Mashariki; na kusimamia maendeleo ya lugha hiyo kwa ujumla;
b) Kusoma miswada, kusahihisha maandishi na kutoa ithibati;
c) Kuteua vitabu vya kutumika mashuleni;

[3] Tazama brosha ya TATAKI 2014/2015, uk. 3

d) Kutafsiri vitabu vya kigeni kwa lugha ya Kiswahili; na
e) Kufanya utafiti katika nyanja za sarufi, kamusi na fasihi na kuchapisha na kusambaza matokeo ya tafiti hizo.

TATAKI (2014/2015) inaeleza kwamba mwaka 1961 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilianzishwa kama Chuo Kikuu Kishiriki cha Chuo Kikuu cha London. Kufuatia hatua hii, Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ilihamishiwa katika chuo hicho kutoka Chuo Kikuu cha Makerere ilikokuwa tangu mwaka 1954. Mwaka 1964 Kamati ilibadilishwa jina na kuwa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili. Mwaka 1970 ikapewa jina la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Mabadiliko haya yalilenga kuifanya Taasisi iwe na sura ya Kiafrika na kuwalenga Waswahili ndani na nje ya Afrika Mashariki kwa mapana zaidi. Hivyo, TUKI ilikuwa na shabaha zifuatazo:

a) Kufanya utafiti katika vipengele mbalimbali vya mofolojia ya Kiswahili, sintaksia, fonolojia, isimujamii na dialektolojia;
b) Kufanya tafiti katika leksikografia na uandishi wa kamusi za Kiswahili na vitabu mbalimbali vihusuvyo lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kibantu;
c) Kuratibu msamiati na kuunda istilahi mpya za maneno anuwai ya kitaaluma;
d) Kuratibu huduma ya kutafsiri matini za serikali na taasisi zake na za viwanda na taasisi binafsi, ndani na nje ya Tanzania;
e) Kufanya tafiti katika fasihi simulizi na andishi na utamaduni nchini Tanzania na Afrika Mashariki;
f) Kushirikiana na asasi nyingine katika kuendeleza lugha ya Kiswahili na kutoa ushauri kuhusu vipengele vya lugha ya Kiswahili na Fasihi;
g) Kuchapisha vitabu na majarida ya Kiswahili kwa ajili ya matumizi ya shule, vyuo na vyuo vikuu; na
h) Kuona kuwa Kiswahili kinakuwa na msingi imara wa kuwa lugha ya kufundishia kuanzia ngazi ya chekechea hadi chuo kikuu.

Wakurugenzi wa TUKI (ambayo baadaye ilibadilika na kuwa TATAKI) tangu kuanzishwa kwake ni hawa wafuatao: G. Mhina (1970 - 1976), A.M. Khamis (1976 - 1982), C.W. Temu (1982 - 1985), D.P.B. Massamba (1985 - 1991), T.S.Y. Sengo (1991 - 1994), S.A.K. Mlacha (1994 - 2000), M.M. Mulokozi (2000 - 2006) na J.G. Kiango (2006 - 2009). Baada ya TUKI kuwa TATAKI, kama tutakavyoona hapo baadaye kidogo, TATAKI imeongozwa na wakurugenzi wafuatao kwa vipindi vifupi vifupi ambao ni: J.G. Kiango, A.K. Mutembei, D.P.B. Massamba na Y.P. Msanjila. Kuanzaia mwaka (2014)a TATAKI inaongozwa na E.S. Mosha.[4]

Mwezi Juni 2009, iliyokuwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Idara ya Kiswahili iliyokuwa chini ya Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ziliungana na kuunda Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Kutoka TUKI, Taasisi hii mpya ya TATAKI imerithi uzoevu wa zaidi ya miaka sabini na mitano ya utafiti kuhusu lugha, fasihi na utamaduni wa Waswahili; na

[4] Imechukuliwa kutoka brosha ya TATAKI 2014/2015, uk. 5-7.

kutoka Idara ya Kiswahili, TATAKI imerithi uzoevu wa miaka kama arobaini ya ufundishaji wa lugha na fasihi ya Kiswahili na usimamiaji wa wanafunzi wa ngazi na viwango mbalimbali. Kuungana huku kunaifanya TATAKI ishughulikie mawanda mapana zaidi kitaaluma ili kukidhi mahitaji ya ukuaji na maendeleo ya lugha na fasihi ya Kiswahili ndani na nje ya Afrika (TATAKI, 2010a: 4).

Tangu mwaka 2009 TATAKI pamoja na kufanya utafiti pia ilianza kufundisha masomo ya Shahada ya Awali (*B.A. Kiswahili*) mwaka 2010, Umahiri (*M.A. Kiswahili*) mwaka 2009. Tangu wakati huo Taasisi imekuwa ikidahili wanafunzi wa Programu za Shahada za Awali na Shahada za Umahiri. Mwaka 2014 Taasisi ilianzisha Programu ya Shahada ya Uzamivu (*PhD Kiswahili*) kwa Tamrini na Tasnifu. Taasisi pia imekuwa ikifundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni huku ikiendelea kuwa Taasisi bora ya utafiti wa maendeleo ya lugha ya Kiswahili duniani.[5] Ili kufanikisha majukumu ya TATAKI ndani ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, TATAKI imeunda Idara kuu mbili: Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu (ILUKII); na Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji (IFAMU). Aidha, vituo vinne vimeundwa kuratibu shughuli za utafiti na ushauri ili kuibua maarifa mapya, na pia kuiingizia Taasisi mapato. Vituo hivi ni: (a) Kituo cha Mapokeo Simulizi na Andishi ya Kiswahili na ya Kiafrika; (b) Kituo cha Istilahi, Tafsiri, Ukalimani na Teknolojia ya Lugha; (c) Kituo cha Sarufi ya Kiswahili na Kamusi (d) Kituo cha Kiswahili kwa Wageni (TATAKI, 2010a: 4). Majukumu ya vituo hivi ni kuratibu tafiti katika uendelezaji na ukuzaji wa Lugha na Fasihi ya Kiswahili.

Yapo mengi sana ya kusema kuhusu historia ya TATAKI tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa. Lakini, haya machache tunadhani yanatosha kwa minajili ya makala yetu ambayo yananuia kujadili mchango wa Taasisi hii katika kukuza na kuendeleza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto ndani na nje ya Tanzania. Ili kujadili vizuri kuhusiana na mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja huu, tunawiwa kutoa historia walau fupi ya fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania. Tutalishughulikia suala hilo katika sehemu inayofuata.

## 4.0 HISTORIA FUPI YA FASIHI YA KISWAHILI YA WATOTO TANZANIA

Nchini Tanzania, "uandishi wa bunilizi za watoto kwa Kiswahili umeanza kupewa umuhimu kuanzia miaka ya 1960, ukapamba moto kidogo miaka ya 1970 na 1980, na kushika kasi zaidi miaka ya 1990" (Mulokozi, katika Semzaba, 2008: iv). Fasihi ya watoto ilipamba moto zaidi katika miaka ya 1990 baada ya Mradi wa Vitabu vya Watoto kuzinduliwa mwaka 1991 (Madumulla, 2001; Mulokozi, 2012). Tangu zamani, fasihi ya watoto iliyokuwa inafahamika katika jamii nyingi za Tanzania na Afrika ya Mashariki kwa kiasi kikubwa, ni ile iliyo katika simulizi, na nyimbo (Omari, 2009) za kitoto za makabila mbalimbali. Katika maeneo mengi, "kazi za watoto kama ushairi, riwaya, tamthilia bado hazijafahamika vyema" (Bakize, 2013: 61).Miaka ya 1990 kulikuwa na juhudi za maksudi za kuinua uandishi na usomaji wa vitabu vya watoto kupitia mashirika mbalimbali kama vile *Canadian Organisation of Development in Education* (CODE), *Canadian International Development Agency*

[5] Imechukuliwa kutoka brosha ya TATAKI 2014/2015, uk. 6

(CIDA), *British Council* na *Agha Khan Foundation*. Baadaye pia, mashirika mengine yaliongeza nguvu kwa mfano, *Book Aid International*, *Pestallozi Children's Foundation* (PCF). Mashirika haya yalisaidia na yanaendelea kusaidia juhudi hizi kupitia Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania. Mradi mwingine uliosaidia kukua kwa fasihi hii ni ule wa TUSOME VITABU uliofadhiliwa na Shirika la *Care International* kwa kusaidia baadhi ya shule kufungua maktaba za vitabu vya watoto.[6]

Kwa upande wa utafiti, nchini Tanzania, hali ya fasihi ya watoto bado siyo nzuri. Utafiti katika eneo hilo ndio umeanza hivi karibuni. Pamoja na maendeleo makubwa ya fasihi hii yaliyowezeshwa na Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania (Mulokozi, 2012), mpaka sasa bado eneo hili linapwaya sana kiutafiti na kiufundishaji. Kwa upande wa uchapishaji, kuna maendeleo makubwa sana. Ripoti ya maendeleo ya Mradi wa Vitabu vya Watoto katika usomaji iliyotolewa na CODE (2015) inaonesha kwamba mpaka mwaka 2015 mradi ulikuwa umechapisha vitabu vya watoto zaidi ya 350 kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hii ni hatua nzuri.

Tukirudi katika upande wa ufundishaji wa kozi ya fasihi ya watoto, hali bado ni mbaya. Ingawa vipengele vya fasihi kama hadithi, methali, na vitendawili vinagusiwa katika fasihi katika shule za msingi na sekondari bado hakuna urasmi wowote wa silabasi unaobainisha kuwa fasihi ya watoto inafundishwa. Vipengele hivyo vinagusiwa tu kidogo na walimu wanapokuwa wanafundisha somo la Kiswahili. Hali hii ni tofauti na jinsi ilivyo huko Kenya ambapo silabasi ya elimu ya msingi na sekondari imebainisha fasihi ya watoto kuwa somo maalumu kabisa. Kwa upande wa vyuo vikuu hali bado hairidhishi vilevile. Kwa mfano, baada ya kozi ya fasihi ya watoto kuanzishwa mwaka wa masomo 2011/2012 katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Bakize, 2013), ni vyuo vichache sana vinavyoendeleza juhudi hizi za kuifundisha kozi hii nchini Tanzania. Kwa taarifa tulizonazo ni kwamba vipengele kadhaa vya fasihi ya watoto hugusiwa tu kwa harakaharaka wakati fasihi ya Kiswahili inapofundishwa. Kozi ya fasihi ya watoto haifundishwi kwa umahususi katika vyuo vikuu vingi nchini Tanzania. Mbali na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mpaka sasa mwandishi alifuatilia na kupata taarifa kwamba vipengele kadhaa vya fasihi ya watoto vinafundishwa ndani ya kozi nyingine za Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge-Moshi, Chuo Kikuu cha Mt. Yohana (Dodoma) na Chuo Kikuu cha Mt. Agustino (SAUT) tawi la Songea tu. Katika ubobezi wa eneo hili, mpaka sasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuna tasnifu 2[7] za Umahiri (zote za mwaka 2016), kuna tasnifu 1[8] ya Uzamivu (ya mwaka 2014), na wanafunzi wawili wanaobobea kwa kiwango cha uzamivu, ambao tafiti zao zinaendelea.

---

[6] http://www.nai.uu.se/ecas-4/panels/141-156/panel-149/Flavia-Aiello-Traore-full-paper.pdf.

[7] Tasnifu ya Umahiri ya Gloria Kimbi yenye mada isemayo, "Dhima ya Takriri ya Kidhamira katika Riwaya za Watoto za Mulokozi" na ya pili ni Tasnifu ya Umahiri ya Bibie Mohammed Nassor yenye mada isemayo, "Dhima ya Taswira katika Hadithi za Watoto: Uchambuzi wa Vitabu vya Hadithi Vinavyosomeshwa Zanzibar."

[8] Hii ni tasnifu ya Uzamivu ya Edith Lyimo yenye mada isemayo, "Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau nchini Tanzania."

## 5.0 MCHANGO WA TATAKI

Kama tulivyodokeza hapo awali, TATAKI inayo historia ya pekee katika kukuza na kuendeleza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania. Ieleweke kwamba tunapoizungumzia TATAKI tuna nia ya kuizungumzia kwa kuihusisha na fasihi ya watoto kama taaluma nchini Tanzania. Ikiwa mtu atazungumzia uchapishaji na usomaji wa vitabu vya watoto Tanzania basi hapo Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania (CBP) unaweza kusimama katika nafasi yake ya kwanza. Hata hivyo, makala haya hayazungumzii suala la usomaji wa vitabu vya watoto. Tunaangazia fasihi ya watoto kama uwanja wa kitaaluma. Kuhusu mchango wa Mradi wa Vitabu vya Watoto katika kukuza na kuendeleza fasihi ya watoto, mwandishi ameandika makala maalumu katika eneo hilo mbali na makala haya. Hivyo, hapa tutaeleza tu mchango wa TATAKI katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Miongoni mwa michango mingine, ifuatayo imeonekana kuwa ya muhimu zaidi:

### 5.1 Mchango kwa Njia ya Ufundishaji

Kama tulivyodokeza katika ikisiri, lengo mojawapo la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni kufundisha ili kutoa maarifa kwa jamii kwa ajili ya kujenga taifa lililo imara kimaarifa. Maarifa hayo hutumiwa katika mambo mbalimbali ili hatimaye taifa liweze kuendelea katika nyanja mbalimbali. Kutokana na mahitaji ambayo hubadilika kila kukicha, mwaka wa masomo 2011/2012, Idara ya Fasihi ya Mawasiliano na Uchapishaji ilianza kufundisha kozi ya Fasihi ya Watoto na Vijana (KF 203). Kutokana na umuhimu wa taaluma ya ualimu katika kufahamu mahitaji ya watoto, ikiwamo fasihi ya watoto, Shule Kuu ya Elimu iliwataka wanafunzi wote wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaosoma Shahada ya Awali ya Ualimu (*B.A. Education*), wanaochukua somo la Kiswahili kama somo la kufundishia, kuhakikisha kuwa wanasoma kozi hii wanapokuwa katika semesta ya pili ya mwaka wa pili wa masomo yao. Aidha, mwaka 2013 ilipoanzishwa Shahada ya Awali ya Kiswahili (*B.A. Kiswahili*) katika TATAKI, wanafunzi wote wanaosoma shahada hiyo, walianza kusoma kozi hiyo kama ya lazima kutokana na mahitaji ya Shahada hiyo. Kutokana na mazingira hayo, ufundishaji wa kozi hii umeendelea kuimarika na kukua zaidi kila mwaka. Mpaka kufikia mwaka 2016, tunaweza kukadiria kwamba zaidi ya wahitimu wa Shahada ya Ualimu 4,000 waliomalizia masomo yao katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, waliokuwa wanachukua somo la Kiswahili kama somo la kufundishia, wamesoma pia kozi ya fasihi ya watoto na vijana.

Huu ni mchango mkubwa kwa taifa kutokana na mahitaji ya mtoto kuzidi kubainishwa na kusisitizwa na Umoja wa Mataifa kila kukicha. Mbali na kusisitizwa na Umoja wa Mataifa, jamii inapofahamu mahitaji ya watoto kielimu na kifasihi, na kuwapatia watoto mahitaji hayo, ni faida kwa jamii husika pia. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba TATAKI imetoa mchango kwa kuwapa maarifa walimu wa Kiswahili ili wawasaidie kifasihi watoto huko mashuleni. Mpaka sasa, TATAKI inaendelea kufundisha kozi hiyo na kila kukicha kozi hiyo inazidi kuboreshwa ili kukidhi mabadiliko yanayojitokeza.

### 5.2 Mchango kwa Njia ya Utafiti

Utafiti katika taasisi ya Chuo Kikuu ndiyo moyo na uhai unaoweza kuifanya taasisi hiyo iendelee kuwapo na kuisaidia jamii na taifa kufahamu na kutatua changamoto au matatizo mbalimbali yanayojitokeza. Aidha, utafiti ni injini ya kuzalisha maarifa mapya na kutathmini yale yaliyopo ili kuwawezesha wanajamii kupata maarifa stahiki kulingana na mabadiliko ya nyakati husika. Katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, pamoja na walimu kuendelea kufundisha kozi ya Fasihi ya Watoto na Vijana (KF 203) kwa miaka 5 sasa, walimu hao, wanafunzi, na wadau wengine wamekuwa wakifanya tafiti mbalimbali zinazozidi kuufanya uwanja huu wa fasihi ya watoto ukue na kuimarika kila kukicha. Matokeo ya tafiti hizo yatazungumziwa baadaye katika kipengele cha mchango wa TATAKI katika uchapishaji. TATAKI imekuwa ikishirikiana na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi, taasisi za kiserikali na watu binafsi, katika masuala mbalimbali ya kitafiti yanayowezesha kukuza fasihi na lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Kwa mfano, kumekuwa na tafiti kadhaa kutoka ndani na nje ya Tanzania zinazolenga kuendeleza fasihi na lugha ya Kiswahili. Aidha, kumekuwa na tafiti kadhaa za fasihi ya watoto ambazo TATAKI imekuwa ikishirikiana na watu wengine, nje ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kupitia walimu wake, na kuzichapisha ili zikuze uwanja huu. Miongoni mwa tafiti za fasihi ya watoto zilizofanywa na wanataaluma wa TATAKI kuanzia mwaka 2009 mpaka sasa ni zile za Omari (2009), Herman (sasa Bakize) (2011, 2012), Mulokozi (2012), Mrikaria (2012), Bakize (2013), Lyimo (2014a; 2014b,) na Bakize (2015). Watafiti wote waliotajwa wanafanya shughuli zao za kitaaluma chini ya usimamizi na uongozi wa TATAKI.

### 5.3 Mchango kwa Njia ya Uchapishaji

Tafiti mbalimbali zikifanywa, hata ziwe nyingi sana, bila kuchapishwa, mchango wake hauwezi kujulikana na wala matokeo hayawezi kuifikia jamii iliyokusudiwa. Pamoja na kufanya utafiti, TATAKI pia ina jukumu la kuchapisha vitabu na matokeo mbalimbali ya tafiti zinazofanyika kwa nia ya kuendeleza fasihi na lugha ya Kiswahili. Lengo hili tulikwisha kulidokeza hapo mwanzo. Hivyo, TATAKI imechangia sana na inaendelea kuchangia katika kuchapisha makala na machapisho mengine kwa ajili ya kuleta maendeleo kitaaluma. Pamoja na machapisho mengine, hapa tutazungumzia zaidi majarida ya TATAKI ambayo ni *Kiswahili*,[9]*Kioo cha Lugha*[10] na *Mulika*.[11] Majarida haya ambayo ni makongwe, yamechangia kwa kiasi

---

[9]*Kiswahili* ni Jarida la TUKI/TATAKI lenye hadhi ya kimataifa kutokana na kukidhi vigezo stahiki. Jarida hilo lilianzishwa tangu Oktoba 1930 likijulikana kama *Bulletin of the ILC*, kisha *Swahili Journal*, likabadilishwa jina na kuwa *Jarida la Kiswahili* mwaka 1969. Limekuwa likichapisha makala kwa lugha nne ( Kiswahili, Kiingereza, Kifaransa na Kijerumani) tangu kuanzishwa kwake mpaka sasa. Jukumu lake kuu, kama yalivyo majarida mengine ya TATAKI, ni kukusanya na kusambaza maarifa yanayohusu Lugha, Isimu na Fasihi ya Kiswahili yaliyokitwa katika utafiti mpevu.

[10]*Kioo cha Lugha*ni Jarida la Kimataifa la TUKI/TATAKI linalochapisha makala ya fasihi na isimu. Jarida hili lilianzishwa mwaka 1995. *Kioo cha Lugha* huchapishwa mara moja kwa mwaka kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Makala juu ya kipengele chochote cha fasihi au isimu, yanayokidhi viwango vya uchapishaji, huwa yanachapishwa.

kikubwa katika kukuza na kuendeleza uwanja wa fasihi ya watoto. Mpaka sasa kuna makala kadhaa yaliyoandikwa na wanafasihi kutoka ndani na nje ya Tanzania.

Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu na kurahisisha ufuatiliaji wa msomaji na mtafiti wa fasihi ya Kiswahili ya watoto, makala haya yaliyochapishwa na majarida ya TATAKI ni haya yafuatayo: “Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania” (Omari, 2009); “Nafasi ya Ubunifu katika Mchezo wa Watoto wa “Michongoano” (Ngugi, 2010); “Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto,” (Herman (sasa Bakize), 2011); “Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya” (Ngugi, 2011); “Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto” (Herman (sasa Bakize), 2012); “*Makuadi wa Soko Huria* (Chachage S. Chachage) katika Muktadha wa Riwaya ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili” (Mulokozi, 2012); “Tafsiri katika Fasihi ya Watoto: Mbinu na Mikakati” (Ngugi, 2012); “Majukumu na Athari za Nyimbo za watoto katika Enzi za Teknolojia ya Kidijitali: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto nchini Tanzania” (Mrikaria, 2012); “Changamoto Zinazoikabili Fasihi ya Watoto nchini Tanzania” (Bakize, 2013); “Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto” (Matundura, Kobia & Mukuthuria, 2013); “Fasihi ya Watoto katika Kutekeleza Mahitaji ya Kisaikolojia ya Mtoto” (Ngugi, 2014); “Nduni za Fasihi ya Watoto ya Kiswahili: Mifano kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania” (Lyimo, 2014); “Gender Balance Struggles in Tanzanian Kiswahili Children’s Literature” (Bakize, 2015); “Mbinu na Mikakati ya Kutumia Fasihi ya Watoto kama Bibliotherapia” (Ngugi, 2015); “Mikakati ya uchambuzi wa Fasihi ya Watoto: Mtazamo wa Upokezi wa Msomaji” (Ngugi, 2016a); na“Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kenya” (Ngugi, 2016b).

Kwa hiyo, kwa ufupi, tangu mwaka 2009 mpaka mwaka 2016, TATAKI imefanikisha uchapishaji wa makala za uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto zipatazo 16. Kuwezesha uchapishaji wa makala 16 katika uwanja mmoja ndani ya miaka 7 si mchango mdogo. Huu ni mchango mzuri unaopaswa kuendelezwa na kupongezwa. Ingawa TATAKI pengine haikuwa ikichapisha, ikiwa na wazo la kuendeleza uwanja huu, basi tunaweza kusema kuwa mafanikio haya ni matunda mojawapo ya ufanisi katika uwajibikaji wa TATAKI katika majukumu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

### 5.4 Mchango kwa Njia ya Uuzaji wa Majarida na Vitabu

Katika jengo la TATAKI, ukienda chumba cha chini kabisa karibu na maegesho ya magari, kuna duka dogo la kuuza machapisho yote ya TATAKI na mengine yanayotoka kwa wachapishaji wengine wanaochapisha kwa nia ya kuongeza maarifa ya fasihi na lugha ya Kiswahili, kutoka ndani na nje ya Tanzania. Majarida yote yaliyochapisha makala tuliyoyataja katika 1.5.3 yanapatikana katika duka hilo. Hata hivyo, ieleweke kwamba yapo majarida pia yanayouzwa pamoja na matoleo

[11]*Mulika* pia, ni Jarida la TUKI/TATAKI lililoanzishwa tangu mwaka 1970 kwa nia ya kuwa daraja kati ya watumiaji wa Kiswahili popote walipo, na wataalamu wa Kiswahili katika Sekondari na Vyuo vya Elimu ya Juu Afrika ya Mashariki. Jukumu lake kuu ni kukusanya na kusambaza maarifa yanayohusu Lugha na Fasihi ya Kiswahili yaliyokitwa katika utafiti mpevu.

yaliyochapisha makala hayo ya fasihi ya Kiswahili ya watoto. Wasomaji wanaohitaji vitabu na majarida mbalimbali huja katika duka la TATAKI kujipatia nakala zao kutokana na mahitaji yao. Mbali na duka hilo, TATAKI yenyewe katika mikakati yake ya kuwafikia wasomaji au wateja, huwa inaamua kwenda katika maonyesho tofautitofauti yanajitokeza katika sehemu mbalimbali ndani na nje ya Tanzania. Katika matukio ya ndani ya nchi, k.m. wakati wa wiki ya utafiti katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kunapokuwa na makongamano ya kitaaluma ndani au nje ya chuo, wakati wa maonyesho ya Saba Saba, huwa TATAKI inapeleka machapisho yake na kuyatangaza. Aidha, TATAKI hutembelea shule za sekondari na vyuo mbalimbali kwa nia ya kujitangaza na kusambaza machapisho yake. Zaidi ya hayo, kuna makongamano mengi nchini Kenya, Uganda na Rwanda ambayo TATAKI imekuwa ikihudhuria kwa nia ya kutangaza machapisho yake. Kwa njia hiyo, wasomaji wanapokutana na makala ya fasihi ya watoto, kwa wale wanaopenda kubobea katika uwanja huo, huwa ni rahisi kupata majarida au machapisho muhimu yanayowafaa. Njia hii nayo inao mchango katika kukuza na kuendeleza uwanja huu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto.

### 5.5 Mchango kwa Njia ya Huduma za Ushauri wa Kitaaluma kwa Jamii

Hapo awali wakati tunataja malengo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, miongoni mwa malengo hayo tulieleza kwamba chuo kinatoa huduma ya ushauri wa kitaaluma kwa jamii katika nyanja mbalimbali. TATAKI kama taasisi inayotekeleza malengo ya chuo imekuwa ikitoa huduma hiyo. Kulingana na malengo ya makala yetu haya, TATAKI imekuwa ikitoa ushauri wa kitaaluma kwa waandishi chipukizi wanaotaka kuandika kazi zao mbalimbali za fasihi na lugha ya Kiswahili. Utafiti wetu umeonyesha kwamba katika mafanikio ya uchapishaji wa vitabu vya watoto, vilivyo chini ya Mradi wa Vitabu vya Watoto Tanzania, wataalamu kadhaa wa TATAKI wamekuwa wakifuatwa na kuombwa ushauri. Ushauri huo umewezesha uandishi na uchapishaji wa vitabu vya fasihi ya Kiswahili ya watoto. Kwa mujibu wa utafiti wa CODE wa hivi karibuni, Mradi umeweza kuchapisha vitabu vya watoto zaidi ya 350 (CODE, 2015). Hivyo, hatusemi kwamba TATAKI imehusika moja kwa moja katika uchapishaji wa vitabu hivyo, lakini taasisi ina mchango kupitia uandaaji wa miswada ya baadhi ya vitabu hivyo. Mbali na ushauri huo wa uandishi, wahadhiri wa TATAKI hasa Prof. J.S. Madumulla, Prof. M.M. Mulokozi, na Prof. K.K. Kahigi wamekuwa wakiwasaidia waandishi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kupitia warsha, semina na makongamano. Kwa mfano, Jestina Naftali mwandishi wa kitabu cha watoto kiitwacho *Gonjwa Sugu* (2011: iii), anakiri kwamba uandishi wa waandishi wengi wachanga katika uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto umekuwa ukiwezeshwa na Prof. M.M. Mulokozi na Prof. K.K. Kahigi kupitia makongamano mbalimbali, likiwamo kongamano la Kibaha, lililohusisha warsha za uandishi miaka ya 2008, 2009 na 2010. Mwandishi anakiri pia kwamba wagwiji hao wa TATAKI, mbali na kutoa semina katika warsha hizo, walikuwa wakiwasaidia waandishi hao wachanga katika uhariri wa kazi zao.

### 5.6 Mchango kwa Njia ya Makongamano

TATAKI imekuwa ikiwawezesha wanataaluma wake kuhudhuria makongamano mbalimbali ya kitaaluma ndani na nje ya Tanzania. Makongamano hayo kwa namna moja ama nyingine yamewezesha TATAKI kujitangaza na kuukuza uwanja huu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Wanataaluma wa TATAKI wamekuwa wakishiriki katika makongamano hayo kwa kuwasilisha makala na kutangaza machapisho ya majarida na vitabu vya taasisi. Kwa mfano, utafiti wetu umebaini kwamba kwa nyakati tofautitofauti TATAKI imekuwa ikiwawezesha wanataaluma kuhudhuria makongamano mbalimbali kama: Kongamano la kimataifa lililofanyika katika hoteli ya Ubungo Plaza tarehe 4-6 Oktoba, 2012; Kongamano la Tisa la Kiswahili na Maendeleo ya Afrika (la CHAKAMA) lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Mt. Agustino (SAUT) Mwanza tarehe 14-16 Oktoba, 2013; Kongamano la Kimataifa la Lugha lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Durban, Afrika ya Kusini tarehe 5-7 Machi, 2014; Kongamano la CHAKAMA lililofanyika katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Rongo, Isbania Kenya, tar. 6-7 Juni, 2014; Kongamano la CHAKITA lililofanyika katika Taasisi ya Kukuza Mtaala, Nairobi, Kenya, tar. 22-25 Oktoba, 2014; Kongamano la Kimataifa la Kiswahili lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Bayreuth, Ujerumani tar. 31 Mei - 2 Juni, 2015 na Kongamano la CHAKAMA la mwaka 2015 lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Mt. Kenya, Nairobi, tar.13-17 Oktoba, 2015. Hiyo ni mifano michache tu ya baadhi ya makongamano ambayo TATAKI imekuwa ikiwezesha wanataaluma wake kuhudhuria. Katika Makongamano hayo yote, ingawa si wanataaluma wote ambao ni wadau wa fasihi ya Kiswahili ya watoto, lakini uchunguzi wetu unaonyesha kwamba katika kila kongamano lililotajwa hapo juu kuna makala moja au zaidi iliyowasilishwa na wanataaluma kutoka TATAKI.

## 6.0 MAPENDEKEZO ZAIDI KATIKA KUENDELEZA FASIHI YA WATOTO

Ingawa tumejadili na kuonyesha mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto yapo mambo kadhaa ambayo tunapendekeza ili uwanja huu wa fasihi ya watoto uzidi kukua zaidi. Mapendekezo haya hayamaanishi kwamba mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja wa fasihi ya watoto ni kidogo. Hoja yetu ni kwamba ikiwa TATAKI imeweza kufanya mambo haya bila kuwa na ajenda maalumu juu ya fasihi ya Kiswahili ya watoto, ikiwa na ajenda mahususi inaweza kufanya makubwa zaidi. Tunaipongeza sana TATAKI kwa mafanikio tuliyotaja na tunaendela kuamini kwamba ikiamua kwa umahususi zaidi inaweza kufanya makubwa zaidi ya hayo iliyoyafanya. Kwa ufupi tunapendekeza yafuatayo:

### 6.1 Kufanyike Kongamano la Kitaaluma la Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

Makongamano ya kitaaluma huwawezesha wanataaluma na wadau wa elimu kukutana, kujadiliana, kubadilishana mawazo na kufanya maamuzi ya masuala kadhaa muhimu ambayo yanahitaji nguvu na juhudi za pamoja. Tunapendekeza

TATAKI iandae kongamano walau hata moja kwa kuanzia ili kuwakutanisha wanataaluma, wadau na wanafunzi mbalimbali wanaoupenda uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Kongamano hilo hata likibeba sura ya Afrika Mashariki, kwa kuwa ndiko kuliko na wazungumzaji zaidi wa Kiswahili, litawawezesha wapenzi wa uwanja huo kubadilishana maarifa na uzoefu. Matokeo ya kongamano kama hilo yanaweza kuwa makubwa. Kwa mfano, wanataaluma watafahamiana na kuanza kufanya miradi au tafiti za pamoja katika uwanja huu. Pili, wanataaluma na wanafunzi wataweza kubadilishana maarifa na uzoefu mbalimbali kuhusiana na uwanja huu. Tatu, wanataaluma na wadau wanaweza kujadiliana na kukubaliana baadhi ya mambo yanayoweza kuusukuma mbele zaidi uwanja huu. Nne, TATAKI itapata fursa ya kutangaza machapisho yake na kuwawezesha washiriki kupata machapisho, hasa ya majarida, ambayo yatawawezesha washiriki kuona tafiti kadhaa ambazo zimechapishwa katika Majarida au Vitabu. Tano, TATAKI itaweza kuchapisha vitabu kadhaa vya makala ya Kongamano katika uwanja huo wa fasihi ya watoto.

### 6.2 Kuendelea kuchapisha Makala na Vitabu vya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

Katika kipengele cha 1.5.3 tuliipongeza TATAKI kwa kuonyesha namna ambavyo imeukuza na kuuendeleza uwanja huu wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kwa njia ya machapisho. Machapisho hayo tumeyabainisha kuwa ni majarida ya miaka mbalimbali kuanzia 2009 - 2016. Kwa ujumla, tumeona kwamba kwa miaka 7, TATAKI imeweza kuchapisha makala 16 ya uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto. Mafanikio hayo yamepatikana bila kuwa na nia maaluma ya kuukuza uwanja huu. Ni mafanikio ambayo yamejitokeza tu kutokana na ufanisi wa kiutendaji wa taasisi katika masuala ya uchapishaji. Hivyo basi, tunapendekeza kwamba kuwe na mkakati maalumu wa kuwahamasisha waandishi wa fasihi ya Kiswahili, wanaopenda, pamoja na kumakinikia maeneo mengine, watafiti na kuchapisha zaidi katika uwanja huu wa watoto. Mbali na uandishi wa makala, TATAKI inaweza kuwamotisha wanataaluma kwa kuwahakikishia kwamba itachapisha chapisho la kitabu au vitabu vyovyote vinavyolenga kukuza uwanja huu. Vitabu hivyo vinaweza vikawa vimeandikwa na mtu binafsi au jopo la waandishi. Pia, TATAKI inaweza kuandaa toleo maalumu la makala ya fasihi ya Kiswahili ya watoto ili kuongeza marejeleo. Waandishi mbalimbali wa makala wanaweza kuandika kutoka kona zote za dunia ya Waswahili halafu TATAKI ikatafuta wahariri wa kuweka kazi hizo vizuri na hatimaye kukapatikana vitabu vizuri.

### 6.3 Kuendelea kuwawezesha Wanataaluma Kuhudhuria Makongamano ya Kimataifa

Kama tulivyoeleza hapo awali katika 1.5.6, TATAKI kwa nyakati tofauti imekuwa ikiwawezesha wanataaluma wake kuhudhuria makongamano ya kitaifa na kimataifa. Hii ni njia nzuri sana ya kuwawezesha wanataaluma kubadilishana uzoefu na maarifa na wanataaluma kutoka vyuo vikuu na taasisi mbalimbali zilizoko nje na ndani ya Tanzania. Kunapokuwa na makongamano ya kitaifa na kimataifa, mara nyingi kunakuwa na uwasilishaji wa makala mbalimbali kutoka kwa wanataaluma. Wakati

huohuo, mara nyingi kwenye makongamano kunakuwa na uuzaji au maonyesho ya kazi mbalimbali za kitaaluma kama majarida, vitabu na machapisho mengine. Yote hayo huwafanya washiriki kupata zana na uzoefu mpya. Njia hii itaendelea kuwawezesha wanataaluma hasa wanaomakinikia uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kujiimarisha kwa kupata maarifa na uzoefu mpya kutoka kwa wenzao wa vyuo vikuu au taasisi nyingine. Hoja kubwa tunayoisisitiza hapa ni kuzidi kuipongeza TATAKI kwa juhudi zake za kuwapeleka wanataaluma kwenye makongamano na kuiomba iendelee na utaratibu huo zaidi kwa manufaa ya kukuza na kuimarisha taaluma katika taasisi na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ujumla.

### 6.4 Kupanua Wigo wa Ufundishaji wa Kozi ya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto

Katika kipengele cha 1.5.1 tulifafanua namna TATAKI inavyochangia katika kukuza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kwa njia ya ufundishaji. Tulieleza kwamba kozi ya KF 203 inafundishwa kwa wanafunzi wa mwaka wa pili wa Shahada ya Ualimu wanaochukua somo la Kiswahili kama somo la kufundishia mashuleni. Pia, kozi hii inasomwa na wanafunzi wa B.A. Kiswahili wanaosoma digrii hiyo katika TATAKI, wanapokuwa mwaka wa pili wa masomo yao. Pendekezo letu ni kuipanua zaidi kozi hii ili isomwe pia kwa kiwango cha Umahiri (hasa *M.A. Kiswahili* kwa Tamrini na Tasnifu) na Shahada ya Uzamivu wa Kiswahili (*PhD Kiswahili* kwa Tamrini na Tasnifu). Kozi hii ikiboreshwa na kuwa na mwendelezo kutoka Shahada ya Awali mpaka kwenye ngazi ya Uzamivu, ni matumaini yetu kwamba watapatikana wanafunzi wengi watakaopenda kubobea zaidi katika uwanja huo. Zaidi ya hayo, machapisho na tafiti mbalimbali katika uwanja huo vitaongezeka.

## 7.0 HITIMISHO

Makala haya yalikusudia kujadili mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza uwanja mchanga wa fasihi ya Kiswahili ya watoto ndani na nje ya Tanzania. Kwanza tulianza kwa kufafanua maana ya fasihi ya watoto, kisha tukaeleza kwa ufupi historia ya TATAKI na fasihi ya Kiswahili ya watoto Tanzania. Baada ya hapo tulifafanua hoja zetu kuhusiana na mchango wa TATAKI katika kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili ya watoto. Katika kiini cha makala tumebainisha kwamba TATAKI imetoa na inaendelea kutoa mchango wake kwa njia ya ufundishaji, utafiti, uchapishaji, uuzaji wa majarida na vitabu, kutoa ushauri wa kitaaluma kwa jamii na kufadhili wanataaluma wa TATAKI katika kuhudhuria makongamano ya kitaifa na kimataifa ndani na nje ya nchi. Pamoja na hayo, tumetoa mapendekezo ya namna ya kuendelea kukuza na kuendeleza uwanja huu wa fasihi. Mapendekezo hayo ni mosi, TATAKI kufanya kongamano au makongamano ya kitaaluma kwa ajili ya kuwakutanisha wanataaluma na wadau wengine wa uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto; pili, kuendelea kuchapisha makala na vitabu vinavyoendeleza uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto; tatu, kuendelea kuwawezesha wanataaluma kuhudhuria makongamano ya kitaifa na kimataifa; na mwisho, kupanua wigo wa ufundishaji wa kozi ya fasihi ya Kiswahili ya watoto mpaka kiwango cha Uzamivu. Tunaamini kwamba mapendekezo yetu haya yakifanyiwa kazi uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya

watoto utakua na kuchukua sura mpya zaidi ya ilivyo sasa. Mwisho, tunamalizia makala yetu haya kwa kuutabiria uwanja wa fasihi ya Kiswahili ya watoto kuwa unaelekea mahala pazuri kutokana na mwitikio mzuri wa wanafunzi, watafiti, wahadhiri na taasisi mbalimbali za vyuo vikuu.

## MAREJELEO


Bakize, L.H. (2013). "Changamoto Zinazoikabili Fasihi ya Watoto Tanzania," katika *Kiswahili*, Juz. 76. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 61-70.

Bakize, L.H. (2015). "Gender Balance Struggles in Tanzanian Kiswahili Children's Literature, katika *Kiswahili*," Juz. 78. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 69-77.

CODE. (2015). "Reading Code**:** Assessing a Comprehensive Readership Initiative in Tanzania," kutoka,www.academia.edu/.../READING_CODE_Assessing_a_Comprehensive_Readershipilisomwa 13/5/2016.

Dube, B. (2004-2006). "Shall the Lamb Feed Together with the Fox? Destroying Race and Gender Stereotypes in Zimbabwean Children's Readers," *Journal of African Children's & Youth Literature*, Juz. 15-16, kur. 17-26.

Herman (sasa Bakize), L. (2011). "Dhima ya Mwingilianomatini kwenye Hadithi za Watoto," katika *Kioo cha Lugha,* Juz. 9. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 73-83.

Herman (sasa Bakize), L. (2012). "Fantasia katika Fasihi ya Kiswahili kwa Watoto," katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 10, Dar es Salaam: TATAKI. kur. 122-134.

Jose, K.A. & Thomas. C. (2007). "Alice & the Cheshire Cat: Children's Literature in the Future," *Journal of Children's Literature*: Children's Literature Association of India. 1(2): kur. 1-4.

Kimbi, G. (2016). Dhima ya Takriri ya Kidhamira katika Riwaya za Watoto za Mulokozi. Tasnifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Lyimo, E.B. (2014a). "Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau nchini Tanzania." Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

Lyimo, E.B. (2014b). "Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto nchini Tanzania," katika *Mulika*, Na. 33, Dar es Salaam: Taasisi za Taaluma za Kiswahili. kur. 33-45.

Madumulla, J. S. (2001). "Hali ya Vitabu vya Watoto katika Tanzania," katika *Kiswahili Forum,* Juz. katika, http://afrikanistik.gko.uni-leipzig.de/swafo/index.php/archives/13-swahili-forum-8-2001, ilisomwa tar. 7/5/2015. kur. 171-183.

Matundura, E., Kobia, J. na M. Mukuthuria. (2013). "Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto," katika *Mulik*a, Na. 32. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 28-47.

Mrikaria, S.E. (2012). "Majukumu na Athari za Nyimbo za watoto katika Enzi za Teknolojia ya Kidijitali: Mifano kutoka nyimbo za watoto nchini Tanzania." Katika S. Omari & G. Mrikaria (Wah). *Mulika.* Dar es Salaam. TATAKI. kur. 75-88.
Mulokozi, M.M. (2012). "*Makuadi wa Soko Huria* (Chachage S. Chachage) katika Muktadha wa Riwaya ya Kihistoria katika Fasihi ya Kiswahili," katika Omari. S na G. Mrikaria (wah.) *Mulika*, Na. 31, Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 51-66.
Muponde, R. (2005). Childhood, History and Resistance: A Critical Study of the Images of Children and Childhood in Zimbabwean Literature in English. Tasnifu ya Uzamivu ya Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Afrika ya Kusini. (Haijachapishwa).
Muponde, R. and P. Stein. (2004-2006). "Mapping the Terrain: Introduction," *Journal of African Children's & Youth Literature*, Juz. 15-16. kur. x-xv.
Naftali, J. (2011). *Gonjwa Sugu*. Dar es Salaam: Kwanza Publishers Limited.
Nassor, M.B. (2016). Dhima ya Taswira katika Hadithi za Watoto: Uchambuzi wa Hadithi Zinazosomeshwa Zanzibar. Tasnifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
Ngugi, P.M. (2010). "Nafasi ya Ubunifu katika Mchezo wa Watoto wa "Michongoano," katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 8. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 67-79.
Ngugi, P.M. (2011)."Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya," katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 9. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 84-94.
Ngugi, P.M.Y. (2012). "Tafsiri katika Fasihi ya Watoto," *Mulika*, 31. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur.12-26.
Ngugi, P.M.Y. (2014a). "Fasihi ya Watoto katika Kutekeleza Mahitaji ya Kisaikolojia ya Mtoto," katika *Kiswahili*, Juz. 77. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur.170-180.
Ngugi, P.M.Y. (2015). "Mbinu na Mikakati ya Kutumia Fasihi ya Watoto kama Bibliotherapia," katika *Kioo cha Lugha*, Juz. 13. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 1-12.
Ngugi, P.M.Y. (2016a). "Mikakati ya uchambuzi wa Fasihi ya Watoto: Mtazamo wa Upokezi wa Msomaji," katika D.P.B. Massamba na L.H. Bakize (wah.). *Kiswahili*, Juz. 79. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 43 - 52.
Ngugi, P.M.Y. (2016b). "Usawiri wa Masuala Ibuka katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Kenya," katika *Mulika*, Na. 35. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 76-86.
Omari, S. (2009). "Fasihi Simulizi na Jinsia: Mifano kutoka Nyimbo za Watoto Tanzania," katika *Kiswahili*, Juz. 71. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. kur. 101-110.
Semzaba, E. (2008). *Marimba ya Majaliwa*. Dar es Salaam: E & D Vision Publishing Ltd.
TATAKI. (2010). *Programu ya Digrii ya M.A (Kiswahili)*. Dar es Salaam: TATAKI.

TATAKI. (2010). *Programu ya Shahada ya Kwanza katika Taaluma za Kiswahili B.A (Kiswahili)*. Dar es Salaam: TATAKI.

TATAKI. (2014/2015). *Brosha ya 2014/2015 ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*. Dar es Salaam: TATAKI.